GAZETI LA KWANZA LA ISLAM KUTOLEWA KWA LUGHA YA KISWAHILI - MWAKA 1936

AHMADIYYA MUSLIM JAMAAT TANZANIA

Mapenzi ya Mungu

MAPENZI KWA WOTE BILA CHUKI KWA YEYOTE

JUZU NO. 238 **Ramdan-Shawwal** 1445 **AH** **Aprili–** 2024 **Shahadat** 1403 **HS** **BEI TSH 800/=**

Mtume Mtukufu[saw] – Mfano Mkuu

'Matukio kutoka kwenye Maisha ya Mtukufu Mtume (saw) – na mwongozo sawa na hali yenye kutisha ya dunia'.

Baada ya kusoma Tashahhud, Ta'awwuz na Surah al-Fatihah, Khalifa Mtukufu, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad (atba) alisema kwamba kuna tukio kutoka kwenye Vita vya Uhud ambapo Mtukufu Mtume (saw) alimuombea dua Hadhrat Sa'd (ra), maombi ambayo yalikubaliwa.

Maombi katika vita kwa ajili ya Hadhrat Sa'd (ra)

Khalifa Mtukufu (atba) alisema Hadhrat Sa'd (ra) aliapa kwamba ama angemuondoa adui au kwamba atauawa kishahidi katika vita. Wakati wa vita, aliona mtu karibu kushindwa na adui, lakini kisha akachukua mawe fulani mkononi mwake na kuyatupa upande wa adui. Hadhrat Sa'd (ra) alipouliza ni nani, aliambiwa kwamba ni Mtukufu Mtume (saw) na kwamba alikuwa akimwita. Kisha Hadhrat Sa'd (ra) akaenda kwa Mtukufu Mtume (saw) ambaye alimweka mbele yake na Hadhrat Sa'd (ra) alikuwa akirusha mishale wakati akiomba. 'Ewe Mwenyezi Mungu, huu ni mshale Wako, na uwapige adui kwa huo.' Mtukufu Mtume (saw) naye alikuwa akiomba, 'Ewe Mwenyezi Mungu, ukubali maombi ya Sa'd. Ewe Mwenyezi Mungu, lifanye lengo la Sa'd kuwa sahihi. Ewe Sa'd, wazazi wangu na watolewe mhanga kwa ajili yako.' Hadhrat Sa'd (ra) alipoishiwa na mishale, Mtukufu Mtume (saw) alimpa mishale yake. Miongoni mwao kulikuwa na mshale ambao haukuwa na makali mbele, hata hivyo, uligeuka kuwa mshale wa kasi zaidi kuliko yote. Inasemekana kwamba siku hiyo Hazrat Sa'd (ra) alipiga mishale elfu moja.



Muhtasari wa hotuba ya Ijumaa ya Hadhrat Khalifatul Masih V[atba] ilitolewa Tarehe 08 Machi 2024

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) amemnukuu Hadhrat Mirza Bashir Ahmad (ra) ambaye anaandika:

Mtukufu Mtume (saw) alikuwa akimkabidhi Sa'd (ra) mishale mwenyewe na Sa'd (ra) angeendelea kuwamwagia adui mshale juu ya mshale. Wakati mmoja, Mtukufu Mtume (saw) alimwambia Sa'd (ra) akisema, "Mama yangu na baba yangu watolewe mhanga juu yako - endelea kurusha mishale!" Hata hadi mwisho wa maisha yake, Sa'd (ra) alikuwa akikumbuka maneno haya ya Mtukufu Mtume (saw) kwa fahari kubwa.' (Maisha na Tabia ya Muhuri wa Manabii (sa) , Juzuu 2, uk. 338)

UK. 11

Jamaat Ahmadiyya yasaidia waathirika Hanang-Manyara

Mwishoni mwa mwaka 2023 baadhi ya maeneo ya kaskazini mwa Tanzania kulitokea mvua kubwa iliyo sababisha mafuriko ya kutisha hususani katika mkoa wa Manyara wilaya ya Hanang-kateshi ambako mafuriko hayo yaliambatana na Maporomoko ya udongo na kusababisha hasara kubwa na maafa ya watu pia nyumba nyingi zilibomoka na nyingine kufunikwa na udongo, barabara zilikatika na adha nyinginezo.



Viongozi mbalimbali wa Taifa akiwemo Mheshimiwa Rais, Waziri mkuu na wengineo walitembelea

UK. 3

Seyyidna Ahmad[as] katika Ramadhani

UK. 03

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

MUSHAWARA

Kuwasili kwa mtukufu Mtume Muhammad (saw) mjini Madina kulileta mapinduzi makubwa kwenye nyanja za kijamii, kisiasa, kiuchumi na Mtume wa Allah aliingia mikataba na makundi yaliyokuwa Madina kwa njia hiyo kukapatikana amani na ustawi.

Hata hivyo mara kwa mara palikuwa panaibuka matatizo na matatizo hayo Mtume wa Allah (saw) alishauriana na Masahaba zake juu ya kuyatatua. Tatizo lililojitokeza na hivyo kuwa la kwanza katika historia ni lile la vita vya Badri. Mtume (saw) alitaka ushauri wao (Masahaba) nini cha kufanya, kwa jazba kubwa walisema sisi hatutakuwa kama wafuasi wa Nabii Mussa (as) waliomwambia Nabii wao aende akapigane yeye na Mola Wake. Wao waliahidi kupigana naye kushoto na kulia na hata kama angeliwashauri wadumbukie baharini wangelikuwa tayari kufanya hivyo.

Wakati wa vita vya Uhudi pia alishauriana na Masahaba. Huu ndio ulikuwa mwenendo wa Mtukufu Mtume Muhammad[saw] na uliendelezwa kwa mafanikio makubwa na makhalifa wake walioongoka.

Akifuata suna na nyayo za Mtukufu Mtume Muhammad (saw), Masihi Aliyeahidiwa (as) daima alishauriana na Masahaba zake, akikutana na mmoja mmoja au wote kwa ujumla. Mfano wa mushawara wa pamoja ulitokea wakati wa Jalsa Salana ya kwanza iliyofanyika Disemba 1891. Kwa sababu Jamaat ilikuwa bado changa na Wanajamaat 75 walikuwa wamehudhuria, haikuonekana ni busara kuwa na mikutano miwili, mmoja ukiwa wa Jalsa salana na mwingine wa Mushawara. Hivyo Masihi Aliyeahidiwa (as) alitumia mkutano wa Jalsa salana kufanyika pia kwa Mushawara. Na kihistoria hii ndio Majlis Shura ya kwanza ya Jamaat. Pendekezo la kwanza lilikuwa kuanzishwa kwa Kamati itakayokuwa na Waahmadiyya na wasiokuwa Waahmadiyya ziandaliwe alama na baraka ambazo zimeteremshwa kwa Jamaat Ahmadiyya na Allah. Pendekezo hili liliwekwa katika kitabu kinachoitwa ***'Asman Faisala'***. Pendekezo hili lilisomwa na Abdulkarim Sialkot baada ya sala ya Adhuhuri tarehe 27 Disemba, 1891. Baada ya hapo wajumbe walitakiwa washauri majina ya wanakamati na watoe maoni kuhusu jinsi kamati hiyo itakavyofanyakazi. Wajumbe ambao walikuja kuzungumzia pendekezo hilo walikubaliana kuwa kitabu kiandikwe na kichapishwe mara moja.

Kama ilivyokuwa kwa Makhalifa waliyoongoka wa Mtukufu Mtume Muhammad (saw), Makhalifa wa Masihi Aliyeahidiwa (as) wameendelea na taasisi hii muhimu ambayo chimbuko lake ni Qur'an Tukufu 42:39 "Na wale waliomwitikia Mola wao na husimamisha Sala, na sheria yao ni kushauriana wao kwa wao na hutoa katika yale Tuliyowaruzuku". Khalifatum Masihi wa pili, Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmood Ahmad (ra) anafafanua kiini na shabaha ya Mushawara katika Jamaat Ahmadiyya. Ni maneno yanayotakiwa kuzingatiwa na wale wanaopewa heshima ya kuwa wajumbe wa Mushawara. Khalifatul Masih wa pili anasema; "Mkutano wetu na utaratibu wetu haukujengwa kwenye misingi inayoongoza mabunge ya dunia au taasisi za kushauriana, kwani wao ni kwamba kila watu wanatetea na kulinda haki zao. Mikutano yao ni kama uwanja wa mapambano ambapo kila mtu na kila upande hutaka haki yake. Lakini sisi shabaha yetu ni tofauti. Na hata utaratibu wetu. Hatukuja hapa kudai haki zetu. Kwani haki zetu zilibainishwa hata kabla ya kuzaliwa. Na hatudai haki zetu kutoka kwa binadamu ambao wana uwezo wa kufanya makosa na wasitupe haki zetu (Report Majlis Shura 1925). Na Khalifatul Masihi wa pili pia anasisitiza; "Tumekusanyika hapa kwa huruma na mapenzi ya Allah ili tuweze kutafakari kuhusu njia ya kueneza nuru na ukweli ulioletwa na Allah kwa ajili ya kuongoza dunia; na tupo hapa kujadili kuhusu masuala ya kijamii na kisiasa ambayo yatajitokeza. Sio kwamba tunataka kupata faida yoyote kibinafsi isipokuwa tunataka kueneza neema kwa binadamu wote.

Kazi ya shura ni kumshauri Khalifatul Masih na ushauri huo utatokana na hofu ya Allah na nia iliyohalisika. Allah Awasaidie wajumbe kutimiza wajibu wao wa kueneza nuru ya Mtukufu Mtume Muhammad (saw).



QUR'AN TUKUFU

2. SURA AL-BAQARA

186. Mwezi wa Ramadhani ambao imeteremshwa humo Qur'an kuwa mwongozo kwa watu, na Ishara zilizo wazi za mwongozo na kipambanuzi. Basi miongoni mwenu atakayeuona mwezi, afunge saumu, na mwenye kuwa mgonjwa au yumo safarini, basi atimize hesabu katika siku zingine. Mwenyezi Mungu Huwatakieni yaliyo mepesi wala Hawatakieni yaliyo mazito, na pia (Huwatakieni) mtimize hesabu na kumtukuza Mwenyezi Mungu kwa kuwa Amewaongozeni, na ili mpate kushukuru.

شَهْرُ رَمَضَانَ الَّذِيْٓ اُنْزِلَ فِيْهِ الْقُرْاٰنُ هُدًى
لِّلنَّاسِ وَبَيِّنٰتٍ مِّنَ الْهُدٰى وَالْفُرْقَانِ ۚ فَمَنْ شَهِدَ
مِنْكُمُ الشَّهْرَ فَلْيَصُمْهُ ۗ وَمَنْ كَانَ مَرِيْضًا اَوْ عَلٰى
سَفَرٍ فَعِدَّةٌ مِّنْ اَيَّامٍ اُخَرَ ۗ يُرِيْدُ اللّٰهُ بِكُمُ
الْيُسْرَ وَلَا يُرِيْدُ بِكُمُ الْعُسْرَ ۖ وَلِتُكْمِلُوا الْعِدَّةَ
وَلِتُكَبِّرُوا اللّٰهَ عَلٰى مَا هَدٰىكُمْ وَلَعَلَّكُمْ تَشْكُرُوْنَ ﴿١٨٦﴾




NUKUU YA HADITHI

عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللهُ عَنْهُ، أَنَّ رَسُولَ اللهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ، قَالَ: «إِذَا جَاءَ رَمَضَانُ فُتِّحَتْ أَبْوَابُ الْجَنَّةِ، وَغُلِّقَتْ أَبْوَابُ النَّارِ، وَصُفِّدَتِ الشَّيَاطِينُ»

Tafsiri:

Imesimuliwa na Hazrat Abu Huraira r.a. ya kwamba Mjumbe wa Allah s.a.w. alisema: Mwezi wa Ramazan uwadiapo, hufunguliwa milango ya Peponi na hufungwa milango ya Motoni, na mashetani hutiwa pingu.
(Sahih Muslim#2495)



Nukuu ya Masih Aliyeahidiwa[as]

Seyyedna Hazrat Masihe Maud[as]. anasema:

"Jambo ambalo ni nguzo ya Islam nayo ni Saumu. Watu hawafahamu ukweli wa saumu…saumu sio hii tu kwamba (mfunga saumu) ashinde na njaa na kiu bali (saumu) ina ukweli wake na athari zake, inayojulikana kwa uzoefu. Na ni asili ya tabia ya binadamu kwamba kadri anavyopunguza kula basi hupata kujitakasa zaidi nafsi na nguvu za kupata kashifu (ufunuo wa Mungu) zinaongezeka."

(Tafsir Hazrat Masihe Maud[as] J.1.UK.258.Chapa mpya)

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Dr. Swaleh Kitabu Pazi
Kompyuta: Jabiri Faraji Bishazo.
Mchapishaji: Sheikh Raghib Zia ul Haq
Msambazaji: Mwl. Omari Ali Mnungu
Wajumbe: 1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Mahmood Hamsin Mubiru.
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu36@gmail.com

Jamaat Ahmadiyya yasaidia waathirika Hanang-Manyara

Kutoka Uk wa 1..



eneo hilo na kujionea hali halisi ilivyo kuwa. Amir sahib Maulana Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry Sahib alimwandikia mheshimiwa waziri mkuu ili kumpa pole kwa janga hilo na kuahidi ya kuwa jamaat itatoa ushirikiano wa kutosha katika kadhia hii. Shirika la Humanity First Tanzania liliwasiliana na wenzao wa Marekani ili kusaidia katika adha hii. Mawasiliano yalifanyika baina ya Jamaat na wizara husika kupitia idara ya majanga na maafa ili kuona ni msaada wa aina gani ambao jamaat inaweza kutoa.

Baada ya kupata mwongozo kutoka idara husika, jamaat kupitia shirika lake la Humanity First ilitoa saruji Tani 30 sawa na mifuko 600 yenye thamani ya zaidi ya Tsh.12, 000,000/= ujumbe wa watu wanne (4) kutoka katika jumuiya ya Ahmadiyya ukiongozwa na mratibu wa shirika la Humanity First hapa nchini Maulana Sheikh Abid Mahmood Bhatti Sahib mkuu wa chuo cha Jamia Ahmadiyya na naib Amir ulitembelea eneo hilo na kukabidhi msaada huo.



Akitoa shukrani nyingi baada ya kupokea msaada huo ,naibu waziri wa ujenzi na uchukuzi Mheshimiwa Godfrey Kasekenya alisema,tunashukuru kwa msaada huu ambao umefika kwa wakati muafaka sawa na mahitaji.Aliipongeza idara ya Humanity First kwa kitendo hicho kizuri na chakupigiwa mfano katika jamii, Akaongeza kusema kuwa "Hakika hili mlilofanya hivi leo na huduma mnazotoa zinaakisi jina la taasisi yenu–yaani ubinadamu kwanza" tunaomba muendelee na moyo huo.

Taarifa za tukio hili zilirushwa na vyombo mbalimbali vya habari kama vile radio,Tv na mitandao ya kijamii.kwa upande wa television,chanel zilizorusha ni pamoja na T.B.C, chanel ten, I.T.V, M.T.A Afrika nk. Kwa upande wa radio ni T.B.C, Radio Ahmadiyya Mtwara nk. Allah ibariki Humanity first, Allah ibariki Ahmadiyya-Amiin.

Seyyidna Ahmad[as] katika Ramadhani

(Sheikh Shahab Ahmad, Arusha)

Saumu ni nguzo muhimu sana katika dini ya kiislamu. Kufunga saumu za Ramadhani kwa kila muislamu. Katika saumu hizi ambaye anavumilia njaa na kiu na anajiepusha na kila aina ya maovu basi moyo wake hupewa nuru maalum inayomsaidia kutekeleza ibada zake vizuri na kuzingatia haki za binadamu wenzake. Vilevile shabaha nyingine ya kufunga saumu ni kuleta nidhamu katika maisha yetu.

Tukitalii maisha matakatifu ya Seyyidna Masihi aliyeahidiwa (a.s) tunafahamu ya kwamba yeye jinsi alivyokuwa anazingatia vizuri ibada ya saumu vilevile alikuwa anafundisha namna ya kujipatia nafasi ya kuzingatia ruhusa iliyotolewa na Qurani tukufu. Katika makala haya hebu tuangalie baadhi ya matukio katika mwezi mtukufu wa Ramadhani.

Dkt Mir Mohamed Ismaily (ra) alikuwa ni rafiki yake na akieleza kuhusiana na saumu za Masihi aliyeahidiwa (as) anasema:

"Mnamo mwaka 1895 ndani ya mwezi mtukufu wa Ramadhani nilipata bahati ya kukaa katika kijiji cha Qadian. Mwezi mzima niliswali sala ya usiku (Tahajjud) pamoja na Masihi aliyeahidiwa (as). Alikuwa na kawaida ya kuswali swala ya witri mara baada ya swala ya isha na Tahajjud aliswali rakaa nane kwa kuunganisha rakaa mbilimbili mwishoni mwa usiku yaani kabla ya swala ya alfajiri.

Kila siku katika rakaa ya kwanza alikuwa anasoma Ayatul kursi (Sura al-baqara aya namba 256) na katika rakaa ya pili alisoma Sura ikhlas (sura namba 112). Na alisoma dua ya **یا حی یا قیوم برحمتک استغیث** katika rukuu na sujda kwa sauti ya juu ambayo hata mimi nilikuwa ninaweza kuisikia.

Pia alikuwa anakula daku baada ya kuswali Tahajud na aliendelea kula daku hadi adhana ya al-fajiri itolewe. Baadhi ya wakati alikuwa anaendelea kula daku mpaka mwisho wa adhana. Kwa sababu baadhi ya wakati huko Qadian adhana ilitolewa katika misikiti mingine kabla ya muda wake wakati bado muda wa kula daku ulibaki. Kwa hiyo Masihi aliyeahidiwa (as) alikuwa anaendelea kula daku hadi mwanga wa asubuhi uonekane upande wa mashariki. Shabaha haswa ya dini ya Islam pia ni hii kwamba watu wasiache chakula mapema sana na waendelee kula daku hadi mwanga wa asubuhi uanze kuonekana upande wa Mashariki. Katika hadithi ya Mtume Muhammad (saw) imesimuliwa kwamba msiache kula daku kwa adhana ya Bilal (ra) bali mwendelee mpaka adhana ya Ibn-e-maktum (ra). Kwa sababu Ibn-e-maktum alikuwa kipofu na hakutoa adhana mpaka watu wengi waseme kuwa tayari kumekucha."

(Siratul Mahdi, Juz. 1, kur. 295-296)

Ingawa katika siku za kawaida pia Masihi aliyeahidiwa (a.s) aliwatunza sana wageni lakini hasa katika mwezi mtukufu wa Ramadhani aliwahudumia sana. Munshi Zafar Ahmad wa Kapurthala anasema:

"Katika Qadian mimi nilikuwa ninakaa chumbani kilichoambatana na Masjid mubarak. Safari moja nilikuwa nikila daku na Masihi aliyeahidiwa aliingia na kusema, kuna kura chapati na mboga ya dengu tu? Wakati huo akamuita msimamizi wa jikoni na kumuuliza kwa nini unawaandalia wageni wetu chakula cha aina moja. Hawa wageni wetu si wasafiri na wanafunga saumu hivyo kila mtu aulizwe anataka chakula gani wakati wa daku ili waweze kufuga saumu vizuri. Baada ya muda mfupi msimamizi wa jikoni akaniletea chakula kingine na wakati huo adhana ilikuwa imeshatolewa lakini Masihi aliyeahidiwa kwamba ningeendelea kula daku kwani adhana ilitolewa mapema kidogo na bado muda ulibakia wa kula daku."

(Siratul Mahdi, Juz. 2, kur. 127)

Munshi Habibu Rahmani akieleza kuhusiana na ugonjwa wa Masihi aliyeahidiwa (as) katika mwezi mtukufu wa Ramadhani anasema:

"Safari moja mimi nilikaa Qadian katika siku kumi za mwisho za mwezi wa Ramadhani. Siku hizo Masihi aliyeahidiwa alikuwa anasumbuliwa na ugonjwa wa kupanda na kushuka kwa homa ya kila siku.

UK. 04

Seyyidna Ahmad[as] katika Ramadhani

Kutoka uk. 3

Mwili wake ulikuwa unatetemeka baada ya wakati wa adhuhuri. Alikuwa anashiriki katika swala ya jamaa wakati wa adhuhuri lakini swala nyingine alikuwa hashiriki. Baadhi ya wakati alikuwa anakaa kabla ya swala ya adhuhuri akiwa anawasubiri watu wengine wanaotaka kuswali. Mimi nilipenda sana kufika karibu naye ili kupata kufahamu anazungumza nini. Safari moja nilimjulia hali na akasema yeye alijisikia baridi na muda mwingine alisema alijisikia baridi sana hata hivyo alifunga saumu. Siku moja nikamuuliza kwamba homa yako sasa imekaa siku kadhaa ni bora ufungue saumu kwani unasumbuliwa sana na maradhi haya. Akajibu kwamba anapata raha wakati wa kufunga saumu na hapati shida. Huwa anapata shida wakati wa usiku ndio maana ni rahisi kwake kufunga saumu wakati wa mchana. Mara nyingi alikuwa hapati homa wakati wa asubuhi kwa hiyo alikuwa anaenda mazoezini baada ya sala ya alfajiri."

(As-hab e Ahmad, Juz. 10, kur. 397-398)

Siku moja baadhi ya watu walitokea Lahore na kuja Qadian ili kuonana na Masihi aliyeahidiwa (a.s). Aliwapokea msikitini na kusalimiana nao na akawaambia marafiki zake wasimamizi wa jikoni kuwatunza vizuri wageni na kuwaandalia chakula wanachokipenda. Mmoja wao alisema kwamba yeye alifunga kwa sababu ya mwezi wa Ramadhani. Hivyo, Masihi aliyeahidiwa alisema kwamba kukubali ruhusa iliyotolewa na Qurani tukufu ni Takwa yaani uchamungu. Mwenyezi Mungu amemruhusu mgonjwa na msafiri kwamba asifunge saumu. Baadhi ya wanazuoni wana mtazamo ya kwamba kufunga saumu katika safari au katika ugonjwa ni dhambi kubwa.
Basi lengo na makusudio ya kufunga saumu ni kupata radhi ya Mwenyezi Mungu na si kufanya upendavyo. Mimi pia sifungi saumu wakati ninaumwa au niko safarini. Kwa mfano nilikuwa sijisikii vizuri ndio maana sijafunga saumu. Kwa sasa nitatoka kidogo nitatembea ili niweze kupata nafuu. Kwa hiyo usione kwamba safari yako haina taabu kwa hiyo unaweza kufunga saumu ukiwa safarini. Quran tukufu haijaeleza mtu apate taabu au asipate taabu katika safari. Saumu haijafardhishwa katika safari.
Ndiyo maana unatakiwa kuzingatia mafundisho kama yalivyo. Basi yule mgeni akaelewa na akasema mimi ninakubali kwa sababu nimekuja kwa Masihi aliyeahidiwa (as) ili kupata mafundisho sahihi na inshallah kuanzia sasa nitafanya hivyo.

(Al-Hakam, 31 Januari 1907, kur. 14)

Miaan Abdullah Sanori anasimulia:
"Muda mrefu uliopita mgeni mmoja alikuja Qadian kwa Masihi aliyeahidiwa katika mwezi wa Ramadhani akiwa ameshinda katika kufunga saumu na muda wa sala ya al-asiri ulikaribia. Masihi aliyeahidiwa akamwambia afungue saumu yake. Akasema muda mfupi ndio umebaki katika kutimiza saumu basi naomba nisifungue na niendelee. Masihi aliyeahidiwa akasema wewe unataka kumridhisha Mwenyezi Mungu kwa mabavu? Mwenyezi Mungu haridhii kwa nguvu ya mtu bali huwa Anaridhia kwa yule anayemtii tu. Kama Ameshasema kwamba msafiri asifunge saumu basi hapaswi kufunga. Hivyo mgeni huyo akafungua saumu yake. "
(Siratul Mahdi, Juz. 1, kur. 97)

Munshi Zafar Ahmad wa Kapurthala anaandika:
"Safari moja mimi, Munshi Arore khan na Muhammad Khan wa Ludhiana tulimwendea Masihi aliyeahidiwa katika mwezi wa Ramadhani nikiwa nimefunga saumu lakini wenzangu hawakufunga. Tulipofika kwa Masihi aliyeahidiwa muda kidogo tu ulibaki hadi kufika kwa muda wa machweo.
Wenzangu wakamwambia Masihi aliyeyahidiwa kwamba mimi nilifunga saumu basi mara moja akaingia nyumbani kwake na akaniletea glasi moja ya juisi ili nifungue saumu yangu kwani haipaswi kufunga saumu katika safari. Mimi nikatekeleza amri yake mara moja na baada ya hapo tulifunga saumu kipindi chote tulichokaa Qadian kama wageni wa Masihi aliyeahidiwa.
Siku moja wakati wa kufuturu Masihi aliyeahidiwa mwenyewe alibeba glasi tatu katika trei kubwa na tukafungua saumu. Nikasema kuwa glasi moja haitamtoshea Munshi Arore khan basi Masihi aliyeahidiwa akatabasamu na akaleta birika kubwa lililojaa juisi na kumwekea bwana Munshi naye akamaliza juisi yote kwa kutazamia baraka za kupata kutoka kwa Masihi aliyeahidiwa mwenyewe."
(As-hab e Ahmad, juzuu 4, uk. 224)

Mke wake Daktari Khalifa Rashid-udin anasema:
"Mnamo mwaka 1903 mimi nilikuja Qadian kutokea Rurki kwa likizo ya siku nne pamoja na marehemu daktari. Masihi aliyeahidiwa (as) aliuliza kama tulifunga saumu katika safari au la na tukamjibu hapana hatujafunga. Akatupangia chumba kimoja nyumbani kwake. Daktari alimwomba Masihi aliyeahidiwa kwamba anapenda kufunga saumu katika siku kadhaa tutakazokaa hapo Qadian. Masihi aliyeahidiwa (as) akasema ni sawa na inshaAllah kila siku nitakuletea chapati za kikashmiri.
Maulvi Abdulkarim wa Sialkot pia alikaa nyumbani kwa Masihi aliyeahidiwa katika orofa ya juu. Wakati wa kula daku mke wake aliyetokea jimbo la Kashmir alikuwa anapika chapati na kutuma kwa Masihi aliyeahidiwa ambaye mwenyewe alikuwa anatuletea katika chumba chetu na alituambia tuendelee kula mpaka kushiba. Sisi tuliona haya jinsi Masihi aliyeahidiwa alivyokuwa anatuhudumia na wakati huo huo tulifurahi pia kwa kupata heshima hii.
Adhana ya alfajiri ilitolewa lakini Masihi aliyeahidiwa alituambia tuendelee kwa sababu bado muda ulikuwapo. Mwadhini amewahi kutoa adhana. Masihi aliyeahidiwa (as) aliendelea kutuhudumia hadi tulishiba. Daktari akamwomba Masihi aliyeahidiwa asijitie taabu kwani sisi wenyewe tutachukua chapati kwa dada wa kazi lakini yeye aliendelea kutusaidia. Kulikuwa na mboga nzuri na tambi zilizopikwa na maziwa pamoja na chakula hicho."

(Siratul Mahdi, Juz. 2, kur. 202-203)

Kwa mujibu wa masimulizi haya tunafahamu jinsi Masihi aliyeahidiwa (as) alivyokuwa anawakarimu wageni. Pia alijitahidi kufunga saumu sawa na uwezo wake hata hivyo alipenda kutekeleza ruhusu zitolewazo na Islam. Mwenyezi Mungu atusaidie kutekeleza ibada ya saumu kwa kuelewa umuhimu wa mwezi wa Ramadhan. Aamin

NUKUU YA LEO

Na.
Ustadhi Issa Malenge.
Ahmadiyya Muslim Jamaat
Tanzania

SAUMU YA MGONJWA.

أَيَّامًا مَعْدُودَاتٍ ۚ فَمَنْ كَانَ مِنْكُمْ مَرِيضًا أَوْ عَلَىٰ سَفَرٍ فَعِدَّةٌ مِنْ أَيَّامٍ أُخَرَ ۚ وَعَلَى الَّذِينَ يُطِيقُونَهُ فِدْيَةٌ طَعَامُ مِسْكِينٍ ۖ فَمَنْ تَطَوَّعَ خَيْرًا فَهُوَ خَيْرٌ لَهُ ۚ وَأَنْ تَصُومُوا خَيْرٌ لَكُمْ ۖ إِنْ كُنْتُمْ تَعْلَمُونَ

Kwa siku zilizohesabiwa. Lakini miongoni mwenu awaye mgonjwa au katika safari, basi atimize hesabu katika siku zingine. Na wale wanaoweza, watoe fidia kwa kumlisha maskini. Na atakayefanya wema kwa radhi ya nafsi yake, basi ni bora kwake; na kama mkifunga ni bora kwenu, ikiwa mnajua (2:185).

Mgonjwa au mtu aliyomo safarini ameambiwa na Mwenyezi Mungu afunge katika siku zingine za afya na baada ya kutoka safarini.

Hali ya ugonjwa ni kiasi cha mtu kujifahamu kuwa yu mgonjwa, basi asifunge; maana akifunga naye ni mgonjwa, amevunja amri ya Mwenyezi Mungu isemayo mgonjwa afunge siku zingine.

Lakini basi mtu anatakiwa kutumia akili pia. Ugonjwa sio maana yake mtu anaumwa umwa kidole au maumivu ya mchoko au udhia mwingine mdogo mdogo.

Ama kwa kutapika saumu haivunjiki isipokuwa mtu ajitapishe kusudi. Wakongwe na wadhaifa wa daima wamepewa ruhusa wasifunge, wakiweza wamlishe maskini mmoja kila siku ya saumu.

Mwanamke mwenye mimba au anayenyonyesha akihofia dhara juu yake au juu ya mtoto, asifunge. Atoe fidia kwa kumlisha maskini kila siku ya saumu au alipe funga katika siku zingine.

Mwanamke mwenye hedhi alipe kwa kufunga siku zingine.

Baadhi ya watu hawana hakika kama katika hali ya saumu mtu anaweza kupigwa sindano au hapana na akipata sindano saumu itasihi au itaharibika. Ukweli wake ndio huu ya kuwa mgonjwa hana saumu. Na ikiwa anaugua kiasi cha kuhitaji kupigwa sindano, basi bila shaka yeye atatakiwa kutii amri na kufuturu hata kama hakupigwa sindano.

Na kama anapigwa sindano si kwa sababu ya maradhi bali kwa satabu nyingine, kama kutaka cheti cha kusafiria (passport),
hata hivyo saumu yake itabatilika kwani dawa

Endelea Uk wa 5..

NUKUU YA LEO

Kutoka uk. 4

inaingizwa mwilini.

Kadhalika damu ikiingizwa mwilini saumu inaharibika vile vile ingawa damu haiingii tumboni, bali mishipani. Hadi ya safari ni ile inayosemwa safari. Watu wengine kwa kukosa kujua husema, safari ya kwa gari na safari ya ndege si safari za taabu na kama mtu katika hali ile afunge saumu si vibaya.

Hii ni kosa, Mtume[saw] amesema, "Si wema kufunga saumu katika safari" [Bukhari].

Mungu hawi radhi kwa kushurutishwa, bali anakuwa radhi yakifuatwa anayoagiza.

Hivyo mtu na awe na raha ya namna gani katika safari lazima asifunge, na akimaliza safari alipe siku alizokula; kwani Mwenyezi Mungu aliyelazimisha saumu ni Mjuzi wa kila kitu, na alijua zitakuwapo safari za raha mbona basi asiseme katika safari za raha mfunge? .

Watu wengine hufunga katika safari wakiogopa taabu ya kufunga peke yao baadaye. Basi wajue ndivyo hivyo alivyowatakia Mungu wawe safarini, ili wafunge saumu huku wakishawishiwa na ulaji wa watu wengine wasiofunga.

Sheria yetu haikatazi watu wasisafiri katika mwezi wa Ramadhan. Bali yameandikwa katika vyuo vya Hadithi kuwa Mtume wetu s.a.w. naye alipata kusafiri mara nyingi katika mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Naam katika safari hizo alikuwa hafungi saumu. Na kama aliondoka kwa ajili ya safari hali ana saumu, basi akifika nje ya mji akafuturu.

Wakati mwingine alikuwa anaagiza kikombe cha maji akayanywa mbele ya watu wote ili wale walio na saumu kati yao wafuturu pia.

Imeandikwa katika ***Sahih Muslim*** ya kuwa siku moja Mtume[saw]. alitoka nyumbani hali amefunga saumu. Alipofika mahali panapoitwa Kura'al Ghamim, umbali wa maili nane, akaagiza maji ya kunywa. Alipoletewa maji ndani ya kikombe alikiinua juu sana ili watu wengine wapate kuona vizuri tendo lake. Kisha akanywa maji hayo hadharani.

Baadaye Mtume[saw]. aliambiwa ya kuwa baadhi ya watu waliokuwa pamoja na Mtume[saw]. hawajafuturu. Kusikia hivi Mtume[saw]. akakasirika na akasema: "Hao ndio waasi, hao ndio waasi."

Ni kweli kuna hadithi nyingine zinazoeleza ya kuwa hata katika hali ya safari mtu anaweza kufunga na saumu yake ikasihi; lakini katika ***Sahih Muslim*** mna hadithi iliyopokelewa na Ibni Abbas, radhi ya Mwenyezi Mungu iwe kwake inayosema ya kwamba desturi ya Mtume[saw]. katika miaka ya mwisho wa uhai ilikuwa kutofunga saumu aliposafiri katika mwezi wa Ramadhan na hii ndiyo desturi iliyoshikwa na Masahaba wote waliopenda kufuata desturi ya mwisho ya Mtume[saw].

Hivyo kufunga saumu katika safari ni kinyume cha desturi (Sunna) ya Mtume[saw]. kama ilivyo kinyume cha maagizo ya Kurani Tukufu.

Naam, ni lazima saumu hizi ambazo hujazifunga kwa sababu ya safari au ugonjwa zilipwe baadaye katika miezi iliyofuata. Na mwenye kuacha kufunga na hali yakuwa anauwezo wa kufunga atapata dhambi.

Kwa mafundisho zaidi tembelea: www.alislam.org

Pichani ni Answarullah Ilaqa ya Dodoma wameshiriki kufanya mahubiri ikiwa ni pamoja na kuuza vitabu na kugawa vipeperushi katika eneo la mnada wa Msalato (maarufu kwa kuuza nyama), takriban kilometa 13 kutoka katikati ya jiji la Dodoma.



Mambo muhimu yaliyojitokeza kwenye mahubiri:

1. Kitabu kidogo cha Sala: Hiki kilionekana kuchangamkiwa zaidi kwani kinaeleza kwa vitendo jinsi ya kupata udhu, namna kusali ikiwa ni pamoja na matamshi ya kwenye kila hatua ya sala. Kinafafanua sala za faradhi, suna, nafali, sala ya Idi, tarawehe n.k, pia ni kidogo kinabebeka kwa urahisi (potable);
2. Kifo cha Nabii Issa[as]: Watu wanashangaa kuwa hivi kumbe Nabii Issa a.s amekufa! Alisikika ustadhi Salum aliyeko kwenye machinjio ya kuku baada ya kukipitia moja ya vipeperushi vyetu. Tulimbainishia hilo kwa kutumia aya za Qurani Tukufu zinazothibitisha kifo cha Nabii Issa[as]. Akakiri kuwa kumbe waislamu hatujui mambo mengi yanayotuhusu. Ustadhi Salum ambaye alionekana kupendezwa sana na mafundisho ya Jamaat ndiye alinunua vitabu vingi zaidi. Akasema akifika nyumbani kwake atatulia na kusoma kwa utuo. Tulimwachia mawasiliano yetu na akatuomba siku nyingine tufike tena mnadani hapo kwa ajili ya kuhubiri. Tulimweleza mahali tunapopatinana na ulipo msikiti wetu hapa Dodoma na kumkaribisha wakati wowote inshallah:
3. Waislamu hatuhubiri dini yetu kama wakristo wanavyofanya: Ustadhi salum ambaye ni maarufu kwa kazi ya kuchinja kuku wanaonunuliwa mnadani hapo, hakuishia hapo bali alionesha masikitiko yake kwa umma wa kiislam ambao hauhubiri dini yao tofauti na wakristo ambao hupenda kuhubiri dini yao mahali popote iwe bar standi ya mabasi n.k wao wanafunga spika na kutangaza "neno". Alitupongeza kwa kazi tunayoifanya ya kutangaza ujumbe wa Islamu. Tulimweleza ustadh Salum kuwa Waislamu wanashindwa kufanya hivyo kwa sababu sio kazi ya waliopewa. Kazi hii ni ya Masihi Aliyeahidiwa a.s ambaye ndiye aliyetumwa hivi sasa kueneza mafundisho sahihi ya Islam, na Waahmadiyya tunaendelea kuifanya kazi hii katika dunia nzima. Hivyo, umma wa kiislam ukitaka uweze kufanya kazi hii (kwa mafanikio) hauna budi kwanza kumpokea Imamu wa Zama.



Bustani ya Washairi

SHANGWE LA RAMADHANI
Shamrashamra, Ramadhani imeshaingia
Nyingi takbira, Mkufunzi tunampokea
Kwa kheri na stara, Rahmani katupendelea
Neema ya dira, Mara tena kuturudishia

Ardhilhali, Mioyoni tulikutarajia
Hombwe idhlali, Dunia tenge melemea
Afua Jamali, Ramadhani umetufikia
Tukwambie hali, Na Manani utatusikia

Tufunge saumu, Kwa juhudu na kwa safi nia
Daku kujihimu, Nafali nuru kujizolea
Mchana timamu, Funga kula kunywa na hisia
Siku ikitimu, Futari na vinono kujifidia

Jama tuifunge, Tena kwa mengi makini
Ndimi tuzichunge, Laghai matusi mdomoni
Nyendo tuzichunge, Amali njema mkononi
Vibwebwe tufunge, Na ibada kuzichuchumia

Kwa tano niage, Kwa hari sisimuzi la roho
Pepo haina bwege, Tia jitihada na mhaho
Takwa tia zege, Stahiki fuzu uvikwe joho
Haya ruka ndege, Ramadhani njema kujivunia

SHUNDA MSHUNDIA WANA
Daluni - Tanga

Mezisikia salamu, zaaina mbalimbali
Sijaipata lotamu, mdomoni kukariri
Kuzidi ya isilamu, yenye maneno mazuri
Salam alaikum, na amani iwe kwenu

Awali hii nidua, kutamka nithawabu
Amani wamtakia, narehema sohesabu
Baraka kurudishia, pale unapoijibu
Salam alaikum, na amani iwe kwenu

Ubaguzi yapingana, matabaka kuepuka
Wote wasalimiana, naheri wakizitaka
Si mkubwa siomwana, salamu itafanana
Salam alaikum, na amani iwe kwenu

Kalamu ninaachia, nawaaga waungwana
Tusiache itumia, Dua tukaombeana
Ubaguzi uchukia, Baraka kutakiana
Salam alaikum, na amani iwe kwenu

Masihi Omary Stambuli Kisagwa

EWE GHAFURU RAHIMU

Ya Ilahi Ya Adhimu, Mfinyanga ulimwengu
Nifanye nikuheshimu, vile upendavyo Mungu
Mno nimejidhulumu, kukubeza Mola wangu
Nisamehe dhambi zangu, Ewe Ghafuru Rahimu.

Tauhidi jambo gumu, la kukupwekesha Mungu
Duni wangu ufahamu, vipi nikwepe machungu
Ya kujivisha sanamu, kuabudu dhati yangu
Nisamehe dhambi zangu, Ewe Ghafuru Rahimu.

Shahada nguzo muhimu, mdomoni kutamka
Kisha kwa wino wa damu, moyoni kuiandika
Sijui na sifahamu, ni lini nitazinduka
Nione nilivyochoka, Ewe Ghafuru Rahimu

Ni lini nitasilimu, nifikie kuokoka
Njia zote za haramu, niweze kuziepuka
Kichwa chapata wazimu, moyo unafadhaika
Nione nilivyochoka, Ewe Ghafuru Rahimu

Dini yataka nidhamu, vyema niishikilie
Tena kwa Istiqamu, dakika nisizembee
Muda, ninajilaumu, ni mwingi unipotee
Mnyonge niangalie, Ewe Ghafuru Rahimu

Imani yanilazimu, Pweke nikutegemee
Tena kwa moyo saliimu, Mola nikusujudie
Mjinga binadamu, mbona nimeshindwa mie
Mnyonge niangalie, Ewe Ghafuru Rahimu

Ole mwana wa Adamu, nimejaa mapungufu
Nimegubikwa maghamu, moyo wangu kama mfu
Vipi nipate stimu, ya kuwa mchangamfu
Ona wangu udhaifu, Ewe Ghafuru Rahimu

Yaa Ilahi Ya Halimu, Mpole Mola Latifu
Mola wangu nirehemu, siku zote nikukhofu
Nikinge Jahannamu, nisisikie harufu
Ona wangu udhaifu, Ewe Ghafuru Rahimu

Moyo wangu ni mgumu, uulinde na ukame
Ukoshe kwa marhamu, kwenye uchafu uhame
Unywe Alif Lam Miimu, ukuabudu kwa shime
Kwa huruma nitazame, Ewe Ghafuru Rahimu

Nipe mbinu maalumu, maasini nisizame
Niishi kitaalamu, kwenda mbele nisikwame
Kigezo changu dawamu, kiwe ni wako mitume
Kwa huruma nitazame, Ewe Ghafuru Rahimu

Ewe mbora Mwalimu, Muwezesha kukhutubu
Ona nisivyo timamu, siko mbali na ububu
Nifanye nitakalamu, kwa maneno ya dhahabu
Sitiri zangu aibu, Ewe Ghafuru Rahimu

Nifunze kwa Ilhamu, mambo nisiyaharibu
Subira niihitimu, niweze kubeba tabu
Mbele ya yangu hukumu, irahisishe hesabu
Sitiri zangu aibu, Ewe Ghafuru Rahimu

Utawa kitu adimu, roho ikiwa legevu
Wapi nipate naimu, inipe ukakamavu
Nakuomba Yaa Karimu, nipunguzie uchovu
Niponye wangu uvivu, Ewe Ghafuru Rahimu

Ewe Uliye Qayyumu, Mola niruzuku nguvu
Unijaze ukarimu, na roho ilo angavu
Nisiisahau zamu, yangu ya kulaza mbavu
Niponye wangu uvivu, Ewe Ghafuru Rahimu

Kila aliye dhalimu, dhambi zake atabeba
Hatompata ghulamu, wala mama wala baba
Dawa pekee i humu, katika kufanya toba
Ikubali yangu toba, Ewe Ghafuru Rahimu

Dunia siishutumu, ila itele misiba
Mola naomba vitamu, vya halali na twayyiba
Ila nishike saumu, kwa njaa au kushiba
Ikubali yangu toba, Ewe Ghafuru Rahimu

Kubaki Muislamu, kwangu iwe ni nadhiri
Kila muda na sehemu, moyoni nikudhukuri
Kwa ari kubwa na hamu, nisizembee amri
Mola wangu nighufiri, Ewe Ghafuru Rahimu

Mengi yangu majukumu, nilinde na ufakiri
Njia Yako nihudumu, bila kuzongwa ghururi
Nikinge na roho ngumu, ninogeshe mahubiri
Mola wangu nighufiri, Ewe Ghafuru Rahimu

Si kwamba najihukumu, wala sifanyi utani
Safari ndefu na ngumu, kila uchao huzuni
Kila ninavyoazimu, pakupenya sipaoni
Oo, Lima sabaqtani, Ewe Ghafuru Rahimu

Ya Ilahi ya Rahimu, Mola wangu niauni
Swiraatwi mustaqimu, nipite kwa umakini
Zisinizonge ithimu, nikaja dondoka chini
Oo, Lima sabaqtani, Ewe Ghafuru Rahimu

Alhaj Sheik Abdulrahman Muhammad. Ame

RAZAKI

Yeye ndo mgawa riziki, Huruzuku kwa mafungu
Pindi tupatapo dhiki, Na kughubikwa machungu
Tusisahau huyu rafiki, Mtibu yote machungu
Nakushukuru razaki, Mtufaa kila hali

Watupa tustahilicho, So kila kile tombacho
Tugawapo bila choyo, Wongeza kipunguacho
Twaafiki unenayo, Na turadhi upendacho
Nakushuru razaki, Mtufaa kila hali

Shunda Mshundia Wana
Daluni, Tanga
+255656557721
Email: shunda267@gmail.com

Wengi wapewe, wanapokuwa na haki
Chache sikizwe, wanapoleta mantiki
Wote wulizwe, mkanganyiko sibaki
Haki tupewe, tusibakiye nachuki

Masihi Omary Stambuli Kisagwa

Unapotaka kutenda, mbili mbili fikiria
Safari kitaka kwenda, barabara ikagua
Uache wako ukinda, fanya Bila kuwazua
Maisha yatakuponda, ukose pakushikia

Masihi Omary Stambuli Kisagwa

Kheri ya siku ya kuzaliwa Mama Samia

Ewe Mungu mpe Samia, Kheri za miaka mia
Kuhudumu kajitoa, Taifa kulinyanyua
Nasi twamfurahia, Na Kazi kuendelea
Neema kwa Tanzania, Twakuomba umuweke

Shunda Mshundia Wana
Daluni - Tanga

Simulizi Yenye Kutia Moyo:

Wewe ni mwenye thamani sana kwa wale wanaokupenda



Msemaji mmoja mashuhuri alianza semina yake kwa kuinua noti ya dola ishirini, katika chumba cha watu mia mbili (200). Msemaji aliuliza, Ni nani angependa noti hii ya dola ishirini ($20)? Mikono ilianza kuinuka. Msemaji alisema, "Nitampa mmoja wenu noti hii ya dola ishirini ($20) lakini kwanza, acha nifanye hivi". Aliendelea kutikisa noti ya dola ishirini. Aliuliza, "Ni nani bado anayetaka?" Bado mikono ilikuwa juu hewani.
Naam, vipi ikiwa nitafanya hivi? Aliitupa chini na kuanza kuiponda sakafuni kwa kiatu chake. Aliinua, sasa ikiwa imechakaa na chafu na kuuliza, "Ni nani anayetaka?" Mikono iliendelea kuinuliwa hewani.
Rafiki zangu, sote tumejifunza somo muhimu sana. Haidhuru ni nini kilichofanywa kwa fedha hizo, bado zilihitajika kwa sababu hazikuwa na thamani iliyopungua. Bado ilikuwa na thamani ya dola ishirini ($20). Mara nyingi katika maisha yetu, tunaangushwa, tunavunjwa na kutupwa matopeni na maamuzi tunayofanya na hali zinazotupata. Huenda tukahisi kana kwamba hatuna thamani na hatuna faida.
Lakini haidhuru ni nini kilichotokea au kitakachotokea, hutapata kamwe kupoteza thamani yako: ukiwa mchafu au safi, ukiwa na kasoro au ukiwa na kasoro ndogo-ndogo, bado una thamani kubwa kwa wale wanaokupenda.

JIFUNZE KUISOMA NA KUIELEWA BIBLIA TAKATIFU NA QUR-ANI TUKUFU:- 28:50--51:

UIELEWE LUGHA YA DINI NA MISEMO YAKE. 14:5 QUR:-

Soma kwa jina la Mola wako Aliyeumba. 96:2; Qur-ani KUSOMA ni AMRI ya Mwenyezi Mungu. KUSOMA ni muhimu na ni lazima kwa mwanadamu yeyote. Na kusoma Kuna njia nyingi na Ina maana Pana sana. Unaweza ukasoma lakini usielewe kile ulichokisoma. Changamoto (MATATIZO) ndio huanzia hapo.

Mwenyezi Mungu hua anaongea kwa misemo mbali mbali, mifano, methali, misamiati, mafumbo nk. Na manabii (MITUME) wake wanafuata nyayo hizo hizo nao hawaongei Kwa matamanio yao, Yoh 6:30 na 53:3--4; Qur an.

Kuna hekima yake Kwa kufanya hivyo. Ili ajue Ni nani anamshukuru na kumkufuru. Ukitumia maarifa (AKILI) vizuri ndio kumshukuru Mwenyezi Mungu. Kwa sababu waliowengi hawataki kutumia AKILI. Ingawa tunakumbushwa. HOSEO 4:6--7; 1wakor 15:34 na 4:83 Qur-ani.

Kwenye Vitabu vya MUNGU Kuna Aya muhkamu na mutashabbihaati. MUHKAM. inatafsili Moja tu. MUTASHABBIHAATI ni kufananisha (MFANO,) Neno Moja linafanana na neno jingine, na inakuwa na maana zaidi ya Moja. Na Aya nyingi sana kwenye Vitabu hivyo ni MUTASHABBIHAATI Zinafananishwa Na zimetumika Kwa mifano, methali, misamiati, mafumbo nk. Tutazibainisha angalau Kwa uchache.

Mwenyezi Mungu ANAONGEA KWA KUFANANISHA AU KWA MIFANO
KUTO 7:1--2; Yoh 10:34--35; NA MANABII (MITUME) WAKE Mt 13:34--35: NA 17:90 Qur-ani tukufu.

Mathayo 13:34--35 na Yoh 6:30; Hayo yote Yesu aliwaambia makutano kwa mifano; wala pasipo mfano hakuwaambia neno; ili litimie neno lililonenwa na nabii, akisema, Nitafumbua kinywa changu kwa mifano, Nitayatamka yaliyositirika tangu awali. (YALIYOSITIRIKA TANGU AWALI ni Yasiyoeleweka maana ya kweli iliyokusudiwa huko nyuma). 2 Petro 3:14-17 vile vile kama katika nyaraka zake zote pia, akitoa humo habari za mambo hayo; katika nyaraka hizo yamo mambo ambayo ni vigumu kuelewa nayo; na mambo hayo watu wasio na elimu, wasio imara, huyapotoa, kama vile wayapotoavyo na maandiko mengine, kwa uvunjifu wao wenyewe.
Basi, wapenzi mkitangulia kujua hayo, jilindeni nafsi zenu, msije mkachukuliwa na kosa la hao wahalifu mkaanguka na kuuacha uthibitifu wenu.

Yeye ndiye Aliyekuteremshia Kitabu, ndani yake zimo Aya Muhkam, zilizo asili ya Kitabu; na zingine mutashaabihaat. Lakini wale ambao mioyoni mwao mna upotofu, basi wanafuata zinazofanana kwa kuitaka fitina na kutamani tafsiri yake (waitakayo); na hakuna ajuaye tafsiri yake ila Mwenyezi Mungu, na wale waliozama katika elimu, husema: Tumeziamini, zote zimetoka kwa Mola wetu; na hawakumbuki isipokuwa wenye akili. 3:8; Qur-ani.

Yuda 1:3-4
Wapenzi, nilipokuwa nikifanya bidii sana kuwaandikia habari ya wokovu ambao ni wetu sisi sote, naliona imenilazimu kuwaandikia, ili niwaonye kwamba mwishindanie imani waliyokabidhiwa watakatifu mara moja tu. Kwa maana kuna watu waliojiingiza kwa siri, watu walioandikiwa tangu zamani hukumu hii, makafiri, wabadilio neema ya Mungu wetu kuwa ufisadi, nao humkana yeye aliye peke yake Mola, na Bwana wetu Yesu Kristo.

6:113--115; Qur-ani tukufu
Na kama hivyo tukamfanyia kila Nabii adui, mashetani

Ukurasa 08

JINSI YA KUPIKA CHAPATI ZA MAJI

MAHITAJI
1. Ngano ½ kilo
2. Mayai 3
3. Mafuta ¼ kikombe
kitunguu kikubwa kilichosagwa 1
4. Kitunguu Swaumu punje 4
5. Chumvi ½ kijiko au zaidi kulingana na matakwa yako



JINSI YA KUPIKA CHAPATI
1. Chekecha unga wako vizuri weka katika bakuli safi.

2. Tia maji katika bakuli la unga na ukoroge mpaka upate uji wa wastani si mzito sana wala si mwepesi sana.

3. Ongeza mayai na chumvi endelea kukoroga.

4. Ongeza kitunguu swaumu na kitunguu maji. Injika kikaango chako jikoni subiri kipate moto.

5. Chota pawa moja mimina na tandaza kuzunguka kikaango subiri sekunde tano hadi kumi mpaka ikauke kisha geuza upande wa pili.

6. Tia mafuta huku ukigeuza na kuzungusha ili mafuta yaenee pande zote na ili chapati isiungue. Endelea kugeuza mpaka iwe rangi ya kahawia.

7. Hapo chapati zitakua tayari kwa kuliwa Fanya hivyo kwa chapati zote zilizobakia.
Chanzo : Facebook Group (JinsiYaKupika)

TANGAZO
Tanziim ya Lajna Imaillah Tanzania

Taanzim ya lajna imaillah Tanzania inapenda kuwatangazia Lajna na Nasrat wote nchini kuwa Ijtmaa ya Lajna na Nasrat 2024 inatarajiwa kufanyika katika eneo la Jamaat Kitonga Dar es salaam tarehe 28 na 29 Juni 2024 ikifuatiwa na Shura siku ya Jumapili tarehe 30 Juni 2024 InshaAllah .

Hivyo Lajna na Nasrat wote wanakumbushwa kufanya maandalizi kwa ajili ya Ijtmaa yetu kama barua ya Ijtimaa inavyoelekeza. Pia wanakumbushwa kuchangia mchango wa Ijtimaa kiasi cha Shilingi 12,000/= kwa Lajna na 3,600/= kwa Nasrat. Allah atujaalie wote tuweze kushiriki ili kufanikisha Ijtmaa yetu InshaAllah

Sadr Lajna Taifa
Zena Nyange.

JIFUNZE KUISOMA NA KUIELEWA BIBLIA TAKATIFU NA QUR-ANI TUKUFU:- 28:50--51:

Kutoka Uk> 07

katika watu na majinni. Baadhi yao wanawafunulia wengine maneno ya ushaufu kuwadanganya, na kama Mola wako
Angalipenda wasingalifanya hayo; basi
waache na wanayoyatunga.

Na ili ielekee kwayo mioyo ya wale wasioamini Akhera, na ili wayaridhie, Na ili wayachume wanayoyachuma. Je, nimfuate hakimu ghairi ya
Mwenyezi Mungu hali Yeye ndiye amewateremshieni
Kitabu kielezacho waziwazi?
Na wale Tuliowapa
Kitabu wanajua kwamba kimeteremshwa na Mola wako kwa haki. Basi usiwe miongoni mwa watiao shaka. (Tusiwe na mashaka kwa ukweli wa maandiko ya Mwenyezi Mungu unapothibitika).

TUNATHIBITISHA
JINSI MANENO HAYO YALIVYOTUMIKA NDANI YA BIBLIA TAKATIFU NA QUR-ANI TUKUFU.

MUHKAM. YOH 17:3 na Sura 112 Qur-ani, Yohana 17:3; Na uzima wa milele ndio huu, Wakujue wewe, Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma.

MUTASHABIHAATI ni kufananisha. (MFANO); MT 6:9; 23:9 na 9:31 Qur-an Mathayo 23:9; Wala msimwite mtu baba duniani; maana Baba yenu ni mmoja, aliye wa mbinguni.(Neno Baba ni mutashabbihaati. Ni Mwenyezi Mungu). Na YESU ni MTU tu Yoh 8:40; TUNAANZA NA TAURATI (BIBLIA TAKATIFU).

BWANA NI mlezi. Mwenyezi Mungu. Taur 4:39; 6:4--5; na kuto 24:1; BABA NI mlezi. Mwenyezi Mungu Mt 6:9; na Mt 23:9; MUNGU AU MIUNGU NI Nabii au Manabii (MTUME AU MITUME) Kutoka 7:1--2; na Yoh 10:34--35;
MWANA WA MUNGU WA KWANZA NI Nabii au Mtume. Kuto 4:22; Zab 89:26--27; Yere 31:9; nk. WANA WA MUNGU NI Wapatanishi au watu wema Mt 5:8--9; NABII (MTUME) NI Mwalimu anaetoka Kwa Mwenyezi Mungu Mt 19:16; ROHO MTAKATIFU NI mpeleka khabali njema Kwa mwanadamu Mt 3:16, Luk 1:19, Luk 2:9--10; MALAIKA GABRIEL (JIBLIIL.) NI mpeleka khabali njema kwa mwanadamu Luk 1:19 na Luk 2:10; MALAIKA NI MTU au watu wema. Luk 20:34--36; Yoh 20:11--12; KUPAA AU KUNYANYULIWA NI kutakaswa, utukufu au Kupewa mamlaka. KUTAHIRI NI KUONDOA GOVI, Uchafu wa mwili na wa Imani Taurati 30:6;

MBINGUNI NI usawa wa kichwa Cha mwanadamu na kuendelea, Hata juu ya mrima ni mbinguni. Kutoka 20:22; 24:18; 19:20;
KUSHUKA AU KUTEREMKA NI Umuhimu na Ubora wa upatikanaji wa MTU, kitu au Jambo Fulani kwa mwanadamu. Yoh 3:13; Yoh 6:38; na 6:41--42; KUSHUKA AU KUTEREMKA MARA YA PILI KWA JINA LILE. NI Ujaji wa Nabii (MTUME) mwingine Kwa HESHIMA ILEILE. Mt 11:13--15 na 17:10--13;

VINAVYOMPA UHAI WA KIMWILI MWANADAMU. MAJINA YAKE YAMETUMIKA KWENYE UHAI WA IMANI. (SHERIA YA MUNGU.) ROHO NI Sheria ya Mungu Hesabu 11:16--18; PUMZI NI Sheria au mafundisho ya mungu mwz 2:7; MAJI NI Neno la MUNGU (Sheria) Amos 8:11; CHAKULA NI Neno la MUNGU (Sheria) Amos. 8:11; NIRA NI kamba. Sheria ya Mungu pia Mt 11:29; SABATO NI Sheria ya mungu au utaratibu anaoutaka Mwenyezi Mungu mwanadamu Aishi. Isa 56:1--4; matendo 15:20--21, nk.

MTI WA MZABIBU NI MTU wa kabira la Israel,
Yoh 15:1--2; MITI YA MIZABIBU NI Watu wa kabira la Wana wa Israel, Isaya 5:1--7; KONDOO NI Kabira la wana wa Israel Mt 15:24; MITI YA MATUNDA MBALI MBALI NI Watu wa makabira mbali mbali tena wenye tabia na Mira tofauti tofauti. mwz 1:11--12; na Mt 7:15--21;

Itaendelea…. Inshallah toleo lijalo

MATUKIO KATIKA PICHA



Pichani ni tukio la kuelekea Maazimisho ya kimkoa ya Masihi Aliyeahidiwa yaliyofanyika huko makao makuu ya Jamaat Ahmadiyya, Dar es Salaam Tanzania pamoja nae Amir Sahib, Maulana Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry



Pichani ni tukio la kuelekea Maazimisho ya Masihi Aliyeahidiwa yaliyofanyika huko Kitonga katika kata ya Msongola, Dar es Salaam



Pichani ni Hayati Al-Haj Ali Hassan Mwinyi na Rais mstaafu wa wa awamu ya pili, akisalimiana na wenyeji wake katika mkutano mkuu wa mwaka wa Jumuiya ya Islam Ahmadiyya huko Kitonga kata ya Msongola, Dar es Salaam mnamo mwaka 2016

JINA ZURI

Na Mwanahistoria wetu.

Mtukufu Mtume Muhammad (saw) ametushauri tuwape watoto wetu majina mazuri. Mzee Ahmad Ismail Mpukutile alizingatia ushauri huo na alipojaaliwa kupata mwanawe wa kwanza akampa jina la Ismail. Kufuatia maombi ya Khalifatul Masih –II, Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmood Ahmad (ra) na malezi ya karibu ya wazazi, Ismail alipata bahati ya kukaa na watu wema na akajaaliwa kutanguliza dini mbele ya dunia, kuenzi na kutumikia Ukhalifa. Kutimiza kwa vitendo masharti ya Baiat yaliyoandikwa na Masihi Aliyeahidiwa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (as).

Ismail Mpukutile alizaliwa Lindi na kutokana na ule msukosuko wa kupiga vita Ahmadiyya baba yake mzazi alihamia Mtama mahali alipopata utulivu na kustawi. Kihitoria Mtama ni mti, na watumwa walikuwa wanapumzika hapo kwenye mti ambao kwa kimwera unaitwa mtama. Hapo walipumzika kupata chakula na hatimaye kuendelea na safari. Kwa Ismail Mpukutile palikuwa ni mahala pa utulivu alipopata fursa ya kutimiza wajibu wake kwa Muumba wake na kutimiza haki za viumbe wake. Kazi yake kubwa ilikuwa kilimo na kazi hii alisaidiana na wake zake wawili. Wa kwanza Bi. Somoe Bakari Nanyembe aliyepata nae watoto wafuatao:- Muhyuddin, Issa, Fatuma, Zainabu na Asha. Na mke wa pili Bi. Somoe Sefu Nakuchima aliyepata nae watoto wafuatao; Rehema, Rukia, Zuhura na Haji. Wote kwa pamoja walisaidiana katika kazi ya kilimo. kilimo chake kikubwa kilikuwa ni bustani, ulimaji wa mbogamboga. Bw. Ismail alitembea sehemu nyingi za nchi akitafuta miche mizuri kwa ajili ya shamba lake. Alikuwa mlimaji mzuri na ndizi za kila aina zilipatikana shambani kwake. Na maofisa walipofika Mtama hususani wale wanaotoka sehemu zinapolimwa ndizi kama vile Mbeya, Moshi, Bukoba aliwaonesha ndizi zake na wakawa wateja wake wazuri. Shamba la mbogamboga likawa la kuvutia hususani kabeji. Masista wa hospitali ya Nyangao walivutiwa sana na bustani hiyo na wakawa wanachukua kabeji kwa ajil ya matumizi ya hospitalini. Mara nyingi walikuwa wanachukua kabeji kwa bili na akawa anafuata pesa baada ya siku mbili tatu. Siku hiyo alifuata pesa ambazo alipewa kwenye bahasha. Alipofika nyumbani alikuta zimezidi na akafunga safari



hadi Nyangao ili kuonana na yule sista amrudishie pesa hizo zilizozidi. Sista huyo alipigwa na butwaa! Na kusema kweli wewe ni Mchamungu. Haraka akawaambia watumishi wa Hospitali wajaze unga, ngano, mafuta ili wapeleke kwa Ismail Mpukutile. Hao waliopewa mizigo hiyo waliombwa watizame hali ya nyumbani kwa bw. Ismail. Mrejesho wa hao watu ni kwamba bw. Ismail anaishi katika nyumba ndogo ilyoezekwa kwa makuti na hii ilizidisha heshima ya bw. Ismail kwani licha ya hali yake ile dhooful hali hakuwa tayari kuchukua mali isiyokuwa yake. Yule Sista alitoa maelekezo kuwa bw. Ismail pamoja na ahali zake wapate matibabu bure pale hospitalini Nyangao. Hayo ndiyo malipo wanayoyapata wanaompokea Masihi wa Mtukufu Mtume Muhammad (saw).

Shamba lake hilo lilimletea faida nyingine. Kutoka pale nyumbani kwake alikuwa anaenda shamabni kwake ambao ni mwendo wa saa mbili. Kwa hiyo alichokuwa anafanya saa ya sala ikifika alikata majani ya migomba na kusali huko huko shambani. Hilo tena likawapa watu neno na kusema Waahmadiyya wachawi. Hofu hiyo ikawafanya wezi wasiguse shamba lake, wakati waliendelea kuiba kwenye mashamba ya jirani zake. Hata hivyo hofu yake kwa Allah ilianza toka ujana wake. Wakati wa ujana wake alikuwa mchezaji mzuri wa mpira. Siku moja kabla ya pambano wachezaji walitakiwa waende kwa mganga. Yeye alikataa katakata. Hakuamini wala kushiriki katika ushirikina. Wachezaji wenzake walimbembeleza sana lakini hakukubali. Toka siku hiyo alipata jina jipya 'Kidini'. Enzi zake zote za mpira na alikuwa mchezaji mzuri aliendelea kuitwa Kidini. Wakati huo huo mfungamano wake na Jumuiyya ya Ahmadiyya na usafi wake wa moyo ikawa ni jambo lililoshuhudiwa na wengi. Bwana Mchora alikuwa na binti yake aliyekuwa na matatizo ya maradhi makubwa, alimuombea na kwa fadhili za Allah binti huyo ni mzima na anafanya kazi hivi leo. Kama tulivyosema mfungamano wake na Jumuiyya ya Ahmadiya ulikuwa mkubwa. Chini ya uongozi akiwa Rais wa Jamaat ya Mtama kwa miaka miwili mfululizo 1977-1978 mkutano wa mwaka Jalsa Salana ulifanyika Mtama. Mafanikio ya mkutano wa kwanza uliofanyika mwaka 1977 yalimvutia Sheikh Jamil Rahman Rafiq aliyekuwa Mubashiri Mkuu wa Jumuiyya ya Ahmadiyya kiasi hiki ya kwamba alishauri mkutano ujao ufanyike tena hapo Mtama. Kishindo cha mkutano wa pili kufanyika Mtama kwa mara ya pili kiliwanyima raha wenye husuda moyoni. Bwana mmoja karibu kabisa palipofanyika mkutano aliendesha zikri ya siku tatu ikipigwa dufu na maombi ya kwamba Ahmadiyya iangamie. Dua la kuku halimpati mwewe! Mkutano ulifanyika na Sheikh Jamil akanogesha zaidi kwa kusema leo mwezi utapatwa. Hapo masheikh walishangilia na kusema uongo na anguko la Ahmadiyya vyote vitatimia leo. Mwezi uliwaka vizuri na Suni huku wakizidi kushangilia na ghafla likatanda giza na mwezi ukapatwa na masheikh wa Mtama wakapata ububu wa ghafla. Kuongeza ufaulu zaidi ile nyumba iliyotumika kwa siku tatu ikipigwa dufu ili Ahmadiyya iangamie ilitafutiwa mnunuzi ainunue wasimpate mnunuzi, mipango ya Allah akainua bw. Saidi Kalindima na kuikabidhi Jumuiyya na hivi leo ni Msikiti wa Jamaat hapo Mtama.

Siku zake za mwisho alitembelewa na nduguye Mchora, alimwita chumbani na kumwambia leo nimeona njozi nikipewa kitabu changu kila nikijaribu kukipokea sikifikii, sasa bwana usimwambie shemeji yako ataanza kulia. Mimi safari yangu i-karibu na kweli baada ya siku tatu alifariki na mazishi yake yaliwavuta wenyeji wengi na kusimamiwa sala ya jeneza na Mwalimu wa Jamati Mwalimu Sembe Sahib.

Mtume Mtukufu^{saw} – Mfano Mkuu

'Matukio kutoka kwenye Maisha ya Mtukufu Mtume (saw) – na mwongozo sawa na hali yenye kutisha ya dunia'.

Kutoka uk. 01

'Msilegee wala Msihuzunike' Khalifa Mtukufu (atba) alisema kwamba wakati Khalid bin Walid alipoongoza kikosi cha Maquraish kwenye kilima ambacho Mtukufu Mtume (saw) alikuwa amesimama juu yake, Mtukufu Mtume (saw) aliomba, na kisha Hadhrat Umar (ra) pia akaleta kikosi kuwageuza. Ilikuwa baada ya haya ndipo Mwenyezi Mungu Mtukufu akateremsha aya ya Qur'an:

Na msilegee wala msihuzunike maana ninyi ndio wenye kushinda kama mu waaminio (Qur'ani Tukufu, 3:140).

Hadhrat Khalifatul Masih V (atba) amemnukuu Hadhrat Mirza Bashir Ahmad (ra) ambaye anaandika:
Wakati Mtukufu Mtume (saw) alipofika kwenye njia ya mlima, kikosi cha Maquraish kinachoongozwa na Khalid bin Walid kilijaribu kupanda mlima na kufanya mashambulizi, lakini kwa amri ya Mtukufu Mtume (saw), Hazrat Umar (ra) alipigana nao pamoja na Muhajirina wachache na wakawafukuza. (Maisha na Tabia ya Muhuri wa Manabii (sa), Juzuu 2, uk. 340)

Khalifa Mtukufu (atba) alisema kwamba licha ya kujeruhiwa yeye mwenyewe, Mtukufu Mtume (saw) alikuwa na wasiwasi kuhusu masahaba wake. Imeandikwa kwamba Hazrat Talha (ra) alionekana akimlinda Mtukufu Mtume (saw) wakati wa vita. Hadhrat Abu Bakr (ra) alipomfikia Mtukufu Mtume (saw) alimkuta amejeruhiwa, hata hivyo, Mtukufu Mtume (saw) alimwambia amchunge Hadhrat Talha (ra) badala yake, kwani alikuwa anavuja damu nyingi.

Khalifa Mtukufu (atba) alisema kwamba baada ya kuwazika mashahidi, Mtukufu Mtume (saw) alirejea kutoka Uhud kwenda Madina. Imeandikwa kwamba Mtukufu Mtume (saw) alirejea Madina kwa wakati kwa ajili ya Sala ya Maghrib. Mtukufu Mtume (saw) alipotoka nyumbani kwake kwa ajili ya Swala ya Maghrib, alihitaji msaada wa kufika msikitini kwa sababu ya majeraha na uchovu wake. Hata hivyo baadaye, ilipofika wakati wa Isha, Mtukufu Mtume (saw) alikuwa amepumzika na alikuwa katika hali nzuri zaidi, hivyo hakuhitaji msaada wowote na aliweza kutembea chini ya uwezo wake mwenyewe.

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) amemnukuu Hadhrat Mirza Bashir Ahmad (ra) ambaye anaandika:
'Baada ya kumaliza shughuli zote muhimu, Mtukufu Mtume (saw) alirudi Madina, jioni ilipokaribia.' (Maisha na Tabia ya Muhuri wa Manabii (sa) , Vol 2, p. 348)

Khalifa Mtukufu (atba) alisema kwamba, kwa maneno mengine, Mtukufu Mtume (saw) hakuondoka mara moja kwenda Madina kwa sababu ya kujeruhiwa, bali alihakikisha kwamba kazi zote muhimu zinashughulikiwa huko Uhud kabla ya kurudi Madina.

Mfano Mtukufu wa Wanawake wa Kiislamu
Khalifa Mtukufu (atba) alisema kwamba wanawake wa Madina pia walionyesha subira na kuridhika. Aliporudi Madina, Mtukufu Mtume (saw) alikutana na Hazrat Hamnah (ra), mke wa Hazrat Mus'ab bin Umair (ra). Alifahamishwa kuhusu kifo cha kishahidi cha kaka yake Hazrat Abdullah bin Jahsh (ra), na kisha akajulishwa kuhusu kifo cha kishahidi cha ami yake. Alikuwa mvumilivu sana na akatamka: 'Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu na kwake Yeye tutarejea.' baada ya kusikia habari hii. Kisha akajulishwa kwamba mume wake pia aliuawa kishahidi, ambapo hakuweza kuyazuia machozi yake. Juu ya hili, Mtukufu Mtume (saw) alisema kwamba uhusiano kati ya mume na mke haufanani na uhusiano mwingine wowote.

Huzur Aqdas (atba) alisema kwamba wakati ndugu, mwana na mume wa Hazrat Hind (ra) walipouawa kishahidi katika Vita vya Uhud. Hadhrat Aisha (ra) alikuwa ametoka kutafuta habari kuhusu Vita vya Uhud. Alimkuta Hazrat Hind (ra) ambaye alikuwa anarudi kutoka Uhud. Alipomwomba habari, licha ya watu watatu wa familia yake kuuawa kishahidi, alisema kwamba Mtukufu Mtume (saw) alikuwa mzima, na kama alikuwa sawa, basi yote yalikuwa sawa. Kisha akasoma aya ifuatayo ya Qur-aan:

Na waliomkufuru Allah Amewarudisha na ghadhabu yao; hawakupata chochote katika heri; na Allah Amewatoshea waaminio katika mapigano. Na Allah ni Mwenye uwezo, Mwenye ushindi kamili. (Qur'ani Tukufu 33:26)

Khalifa Mtukufu (atba) alisema kwamba Hadhrat Hind (ra) alikuwa akiichukua miili ya marehemu ya familia yake juu ya ngamia wake kuelekea Madina. Hata hivyo, ngamia alikuwa hasogei alipokuwa akielekea Madinah bali alisogea kwa haraka huku akimuelekeza upande wa Uhud. Alirudi Uhud, akakutana na Mtukufu Mtume (saw), na akasimulia tukio hili kwa Mtukufu Mtume (saw). Mtukufu Mtume (saw) aliuliza iwapo mume wake alikuwa amefanya kiapo chochote kabla ya vita, na akajibu kwa kusema kwamba aliahidi kutorejea kwa watu wake akiwa amefedheheka na aliomba kuuawa kishahidi katika vita. Mtukufu Mtume (saw) alisema kwamba hii ndiyo sababu ya ngamia kutosogea kuelekea Madina. Mtukufu Mtume (saw) alisema kwamba baadhi ya watu ambao, kama wanasema jambo, huku wakiapa kwa Mwenyezi Mungu, basi Mwenyezi Mungu hulitimiza, na Amr bin Jamuh (ra) alikuwa miongoni mwa watu hao. Kisha mashahidi wa Uhud walizikwa huko Uhud.

Khalifa Mtukufu (atba) alisema kwamba ataendelea kusimulia matukio haya katika siku zijazo.

Wito wa Maombi kwa ajili ya Wapalestina, Hali ya Kutisha ya Ulimwengu na Waahmadiyya huko Yemen.

Khalifa Mtukufu (atba) alihimiza maombi kwa ajili ya Wapalestina. Mwenyezi Mungu Mtukufu awafanyie wepesi. Kama matokeo ya mawazo na matendo yao potovu, maadui wamedhamiria kuwaangamiza. Badala ya kujaribu kusimamisha vita, mataifa makubwa yenye nguvu yanajaribu kuwasha moto. Rais wa Marekani alitoa wito wa kusitishwa kwa mapigano wiki iliyopita, na sasa inasemekana usitishaji vita utafanyika kabla ya Ramadhani, lakini kwa muda wa wiki sita tu. Yote hii itafanywa ili kuwapa Israeli muda wa kupumzika na kisha kuanza ukatili wao upya. Hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu ndiye awezaye kuwakomesha. Kwa hivyo, lazima tuombe. Kupitia misaada, Waahmadiyya wanapaswa kujaribu kuwapa chakula, dawa au aina yoyote ya msaada. Katika maeneo yao, wanapaswa pia kupaza sauti zao kwa ajili ya kukomesha dhuluma hizi. Waendelee kuwaandikia barua wanasiasa na wasichoke kufanya hivyo. Mwenyezi Mungu Mtukufu awawezeshe Wapalestina nao wazidi katika sala na maombi yao na kuboresha hali zao za kiroho.

Pia kuna habari kwamba Ulaya na Marekani zitahusika moja kwa moja katika vita vya Russia na Ukraine na hii pia inaongeza tishio la vita vya dunia. Kwa hiyo, ni lazima tuombe kuhusu jambo hili pia; Mwenyezi Mungu Mtukufu ailinde dunia na maangamizo. Khalifa wa Nne (rh) alikuwa ameagiza dawa ya homeopathic kusaidia kulinda dhidi ya athari za atomiki na kila mtu anapaswa kukamilisha matumizi ya dawa hii. Waahmadiyya pia wanapaswa kuhifadhi chakula kwa angalau miezi miwili hadi mitatu majumbani mwao. Hata ikiwa hakuna vita, kuhifadhi chakula kunaweza kuwa na manufaa.

Khalifa Mtukufu (atba) pia alihimiza maombi kwa ajili ya Waahmadiyya wa Yemen; Mwenyezi Mungu Mtukufu afanye upesi njia za kuwaachilia huru. Kuna kundi la Wayemen linadai kuwa Waahmadiyya wanapanga njama dhidi ya serikali; Mwenyezi Mungu Mtukufu aziondolee fikra hizi na awatafutie njia za kuwaachilia Waahmadiyya.

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) aliomba kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu aujaalie ulimwengu hekima, kwamba badala ya kutumbukia katika maovu ya dunia kwa kivuli cha maendeleo, wamtambue Mwenyezi Mungu Mtukufu. Mwenyezi Mungu Mtukufu aziwezeshe nchi za Kiislamu kusimamisha uadilifu na kuwa na umoja. Mwenyezi Mungu Mtukufu atuwezeshe kufikisha ujumbe wake kwa kila mtu duniani.

Mwendelezo wa Hotuba hii unapatikana katika vituo vyote, kwa njia ya mtandao na Karatasi.

The First Muslim Newspaper in Swahili Language since 1936

Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania

Mapenzi ya Mungu

MAPENZI KWA WOTE BILA CHUKI KWA YEYOTE

HABARI UK> 10

JINA ZURI



HABARI UK> 8

TANGAZO

Kuelekea Ijitimaa ya Kitaifa Lajna Imaillah Tanzania

MBUYU UMEANGUKA

Na Mwanahistoria wetu.

Katika tamthilia maarufu ya William Shakespeare, ambayo Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ameitafsiri kwa Kiswahili; ***"Julius Kaisari"***. Shakespeare anasema; ***"Maovu wayatendayo binadamu huishi wakishakufa, mema huzikwa nayo"***. Hiyo haikuwa hivyo kwa Alhaji Alli Hassani Mwinyi. Tuliyobaki tunaendelea kusimulia hadithi njema ya maisha yake na kuna uwezekano kuendelea kusimulia hadithi hiyo kwa miaka mingi ijayo, Insha Allah.


Sifa anazopewa Alhaji Alli Hassani Mwinyi hakuna chumvi ndani yake. Anastahili. Ni kweli alikuwa Mbuyu na mbuyu ukianguka panatokea athari kubwa. Alikuwa ni Maktaba. Ni kweli safari ya wazazi kutoka Kivule hadi Mangapwani akakulia huko akapata malezi, akapata elimu nje na ndani ya nchi, kuwa Katibu Mkuu, kuwa Balozi, kuwa Waziri, Rais wa Zanzibar, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mwenyekiti wa CCM, yote haya yanampa nafasi ya kweli kuwa Maktaba. Na hatutakosea tukisema Maktaba imefungwa. Lakini wale ambao hawakufanikiwa kuingia katika Maktaba hiyo nadhani wanaweza kuambulia kidogo maktaba hiyo kwa kusoma; **"Mzee Rukhsa Safari ya Maisha yangu"**.

Hapana shaka yoyote Mwinyi alikuwa ni mtu rahimu, mnyenyekevu, mcha Mungu, kiburi ilikuwa ni desturi iliyokuwa baidi kabisa na khulka yake. Alitukanwa lakini hakurudishia. Yeye alijiona kichuguu na mema yote tulifanya sote lakini mabaya alifanya yeye! Hapa inahitaji tafakuri. Njia pekee ya kukumbuka neema hii aliyopewa ya miaka 98 ni sisi kujitahidi kuwa vichuguu na kutupandisha mabega. Kujiuzuru, kuacha kitumbua ni mwiko katika siasa za Afrika. Mtu atang'ang'ania wee kufa na kupona. Atajaribu hata kubadili katiba. Mwinyi alionesha njia. Yeye alitengua kitengdawili hicho na akajiuzuru uwaziri wa mambo ya ndani si kwa sababu alifanya kosa. La hasha! Cheo ni dhamana na bila shaka utaulizwa katika amana ulizopewa. Yeye alijiuzuru kwa sababu wale walio chini yake hawakutimiza wajibu wao.



Mwinyi hakuvumilia maumivu ya watu na hili lilihitaji ushujaa na ujasiri. Wakubwa, Mashailoko wa dunia walikuwa wanataka kipande cha mnofu. Akiwa na David Msuya Waziri wa fedha wakati huo akazungumza nao milango ikafunguliwa na tukapata soko huria. Bila shaka unapofungua dirisha dhamira ni hewa lakini nzi anapita hapo hapo na siajabu hata wezi. Kwa vyovyote milango ikafunguliwa, uhuru ukaongezeka magazeti yakashamiri, vyama vingi vikaanza kazi, haki za binadamu zikawa sehemu ya katiba, kila mtu akatakiwa kutimiza wajibu wake, kuwa katika mipaka, kuabudu sawa na imani yake, kutomchagulia chakula mtu, lakini yote hayo yafanyike katika mipaka inayokubaliwa. Upepo huu ndio uliyompatia jina 'Rukhsa' iliyoiwezesha nchi kupumua.

Kama ukitaka kujifunza mila, desturi na utamaduni wa Kiswahili njia ni kumsikiliza Mwinyi. Mapenzi yake kwa Kiswahili yalikuwa makubwa. Kwa miaka aliongoza baraza la Kiswahili. Umahiri wake wa kuchagua maneno ulikuwa mkubwa. Staha za Uswahilini ilikuwa ni hazina yake. Katu hakuchanganya Kiswahili na Kingereza kama wanavyofanya kinafulani. Dibaji aliyoiandika kuhusu ushairi katika kitabu cha **'Amir Sudi Andanenga' - *Bahari ya elimu ya Ushairi*** ni ushairi wa mapenzi makubwa aliyo kuwa nayo kwa lugha ya Kiswahili. Tutafanikiwa kumuenzi kama tutafanya kila kinachowezekana ili kuendeleza lugha yetu ya taifa Kiswahili.



Hakika ya Ahmadiyya
(The Truth of Ahmadiyyat)
By Hadhrat Mirza Bashir-ud-Din Mahmood Ahmad r.a. Khalifatul Masih II
(Swahili translation).

This book was first published as a lecture delivered by Khalifatul Masih II r.a. on 31st October 1948 at Sialkot Pakistan and appeared in Al Fazl newspaper in Urdu language.

Due to its importance in establishing the true picture and removing all doubts about the message of Ahmadiyyat, it was translated into Swahili language by Maulana Sheikh Mubarak Ahmad.

The book covers shortly but precisely about:
The Beliefs of Ahmadiyyat in different controversial matters.
The need of establishing new Jamaat.
Systems of Jamaat Ahmadiyya in Preaching Islam and Changes which have already occurred as the effect of the teachings of Ahmadiyyat.

AHMADIYYA MUSLIM JAMAAT TANZANIA


HAKIKA YA AHMADIYYA

Hadhrat Mirza Bashir-ud-Din Mahmood Ahmad r.a. Khalifatul Masih II

JUMUIYA YA WAISLAMU WA AHMADIYYA TANZANIA

Nakala hii itapatikana kwa Tsh. 950/=

Je, Wajua?

Hewa ya carbondioxide inatumika kuondoa hewa ya oxygen. Poda au mapovu hutumika pia kufunika eneo linalowaka moto ili kufanya hewa ya oxygen isifikie kitunachoungua, hivyo kufanya moto uzimike.

Kwa Makala, Maoni, Ushauri; Tuandikie

mapenziyamungu36@gmail.com